AMRI KUMI ZA MUNGU

Darasa la 2

la watoto

by Denis & Devis Julius

DARASA LA PILI.

Huu ni mfufulizo wa mwongozo wa madarasa ya watoto. Kama mwalimu/mzazi ikiwa hujapata sehemu ya kwanza. Basi wasiliana nasi kwa namba zinazoonekana chini ya makala hii, upate sehemu ya kwanza.

Darasa hili la pili linahusu Amri kumi za Mungu. Ni darasa la mwezi mzima. Hakikisha unawakutanisha walau mara mbili (2) kwa wiki, na kuwapa mazoezi ya kila siku, ili maneno hayo yakae kichwani kwa haraka zaidi. Rika la wanaostahili darasala hili ni kuanzia mwaka 0-12, Kumbuka mtoto anashika kwa haraka zaidi ya mtu mzima. Hivyo wajazie maarifa ya Neno la Mungu haraka, kabla shetani hajawajazia yake.

Mithali 22:6
[6]Mlee mtoto katika njia impasayo,
Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee.

AMRI KUMI (10), NI NINI?

Mwl: Amri kumi ni nini?

Mtoto: *Ni maagizo ya upendo tulioagizwa na Mungu tuyatende kama sharti, sikuzote zote za maisha yetu.*

Mwl: Je amri 10 zinapatikana katika kitabu gani kwenye biblia?

Mtoto: *Kitabu cha Kutoka sura ya ishirini, mstari wa kwanza hadi wa kumi na saba (Kutoka 20:1-17).*

Mwl: Zitaje zote.

Mtoto:

Amri ya 1:

Mimi ni BWANA, Mungu wako, niliyekutoa katika nchi ya Misri, katika nyumba ya utumwa. Usiwe na miungu mingine ila mimi.

Amri ya 2:

Usijifanyie sanamu ya kuchonga, wala mfano wa kitu cho chote kilicho juu mbinguni, wala kilicho chini duniani, wala kilicho majini chini ya dunia. Usivisujudie wala kuvitumikia; kwa kuwa mimi, BWANA, Mungu wako, ni Mungu mwenye wivu; nawapatiliza wana maovu ya baba zao, hata kizazi cha tatu na cha nne cha wanichukiao, nami nawarehemu maelfu elfu wanipendao, na kuzishika amri zangu.

Amri ya 3:

[7]Usilitaje bure jina la BWANA, Mungu wako, maana BWANA hatamhesabia kuwa hana hatia mtu alitajaye jina lake bure.

Amri ya 4:

Ikumbuke siku ya Sabato uitakase.
Siku sita fanya kazi, utende mambo yako yote; lakini siku ya saba ni Sabato ya BWANA, Mungu wako, siku hiyo usifanye kazi yo yote, wewe, wala mwana wako, wala binti yako, wala mtumwa wako, wala mjakazi wako, wala mnyama wako wa kufuga, wala mgeni aliye ndani ya malango yako.
Maana, kwa siku sita BWANA alifanya mbingu, na nchi, na bahari, na vyote vilivyomo, akastarehe siku ya saba; kwa hiyo BWANA akaibarikia siku ya Sabato akaitakasa.

Amri ya 5:

Waheshimu baba yako na mama yako; siku zako zipate kuwa nyingi katika nchi upewayo na BWANA, Mungu wako.

Amri ya 6:
Usiue.

Amri ya 7:

Usizini.

Amri ya 8

Usiibe.

Amri ya 9:
[16]Usimshuhudie jirani yako uongo.

Amri ya 10:

Usiitamani nyumba ya jirani yako, usimtamani mke wa jirani yako; wala mtumwa wake, wala mjakazi wake, wala ng'ombe wake, wala punda wake, wala cho chote alicho nacho jirani yako.

Mwl: Je Amri kumi zimegawanyika katika makundi mangapi?

Mtoto: *Makundi mawili.*

Mwl: Yataje.

Mtoto: *Amri za upendo kwa Mungu wetu na Amri za upendo kwa jirani zetu.*

Mwl: Amri za upendo kwa Mungu zipo ngapi na zitaje

Mtoto: *Zipo nne nazo ni…(Anataja)*

Mwl: Amri za upendo kwa jirani zetu ni ngapi, zitaje

Mtoto: *Ni sita.. nazo ni.(anataja)*

Mwisho wa sehemu ya kwanza

Kama mwalimu zingatia kurudia- rudia kumfundisha azitaje mpaka zikae kichwa na kuweza kueleza migawanyiko hiyo kiufasaha. mjengee nidhamu ya umakini, wala usiruhusu, michezo mingi ili apate nafasi ya kuziweka amri hizo haraka kichwani. Upate nafasi ya kuendelea darasa jingine. Darasa hilo utaenda nalo kwa wiki mbili.

Sehemu ya pili:

Mwl: Je tumejuaje kuwa amri kumi zimegawanyika katika makundi hayo na kwamba ni maagizo ya upendo na sio sheria?.

Mtoto: *Bwana Yesu alizifafanua vema katika kitabu cha Mathayo 22:35-40*

Mwl: Alisemaje?

Mtoto: *Mathayo 22: 35-40*

Mmoja wao, mwana-sheria, akamwuliza, akimjaribu; Mwalimu, katika torati ni amri ipi iliyo kuu? Akamwambia, Mpende Bwana Mungu wako kwa moyo wako wote, na kwa roho yako yote, na kwa akili zako zote. Hii ndiyo amri iliyo kuu, tena ni ya kwanza.
Na ya pili yafanana nayo, nayo ni hii, Mpende jirani yako kama nafsi yako. Katika amri hizi mbili hutegemea torati yote na manabii.

Mwl: Je tutawezaje kufanikiwa kumpenda Mungu?

Mtoto: *i)Kwa kupenda kujifunza biblia*
ii) Kwa kupenda Kuomba,
iii)na kuhudhuria ibadani

Mwl: Ni thawabu gani mtoto anazipata kwa Mungu anapozishika amri zake?

Mtoto: *Mungu atampenda na kujidhihirisha kwake.*

Mwl: Je Neno hilo limeandikwa wapi kwenye biblia?

Mtoto: *Anataja.*
Yohana 14:21
Yeye aliye na amri zangu, na kuzishika, yeye ndiye anipendaye; naye anipendaye atapendwa na Baba yangu; nami nitampenda na kujidhihirisha kwake.

Mwl: Kati ya amri 10, ni ipi? yenye ahadi kwetu sisi watoto.

Mtoto: *Amri ya tano*

mwl: inasemaje.

Mtoto: *(anataja)*

Mwl: Je tunamuheshimuje mzazi?

Mtoto: *i) Kwa kumtii pale anapotuagiza.*
ii) Kwa kumsikiliza na kutendea kazi pale anapotufundisha.
iii) Kwa kutorudia makosa pale anapotuadhibu.

Mwl: Je! tunaombaje? ili Mungu atusaidie kuzitii amri za Mungu?

Mtoto: *Asante Bwana Yesu kwa kunifundisha amri zako, nisaidie niweze kuzikumbuka na kuzishika, sikuzote za maisha yangu. Amen.*

******MWISHO*****

Kama mwalimu/ mzazi. Darasa hili la amri kumi litamjengea mtoto kuyajua maagizo ya Mungu hivyo ukiisha mfundisha hakikisha sasa unamwonyesha

kimatendo, isiwe tu kukariri… pale anapoonyesha kutosikia unamwambia unakumbuka amri ya tano inasemaje? waheshimu Baba yako na mama yako.

Anapokataa kwenda kwenye mafundisho ya biblia, unawakumbusha amri ya upendo kwa Mungu inasemaje?

Vilevile unaanza kumpa mazoezi ya upendo. Unampa majukumu ya kumtendea/mazazi mlezi wake, kisha ajapo kwenye mafundisho unamuuliza alitekelezaje.

Mweleze madhara ya kusema uongo, madhara ya udokozi, kwamba vyote hivyo vinaenda kinyume na zile amri kumi tulizojifunza.

mpe nafasi ya kuuliza maswali, mjibu. Mfundishe nyimbo za upendo, na thawabu mtu azipatazo kumtii Mungu. Zitamwongezea shauku zaidi.

Lakini pia mtie moyo kuwa akizishika amri atakuwa mpenzi wa Mungu na hivyo Mungu atajifunua kwakw sana.na atapendwa na watu wote kama Samweli.

Mjenge hapo, kimatendo huku ukimkumbusha alichokikariri. Na Bwana atatenda ndani yake kwa yaliyosalia.

Fanya hivi kwa mwezi mmoja mzima.

Bwana akubariki.

Mwendelezo wa darasa la 3 unakuja….

KWA MAWASILIANO

Mch. Denis &Devis Julius
Nuru ya Upendo wa kristo
Piga/Whatsapp: +255 693036618/ +255 789001312
www.wingulamashahidi.org
info@wingulamashahidi.org